*Mulika, Na. 42 (1), 125-137*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Athari za Kimsamiati za Mtagusano wa Jamii-Lugha ya Waswahili na Jamii-Lugha Nyingine za Kigeni

*Musa Mohamed Salim Shembilu*[1]
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na42t1.8

**Ikisiri**

Kiswahili kimekuwa ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi ndani na nje ya Bara la Afrika. Katika kukua huko kimetagusana na jamii-lugha nyingine za kigeni kama vile Kiarabu, Kireno, Kijerumani, na Kiingereza. Zipo jamii-lugha zilizotagusana na Kiswahili kutokana na sababu za kiutawala kama vile Kiarabu, Kijerumani na Kiingereza. Zipo pia zilizotagusana kwa sababu za kijamii ambazo ni kama vile Kihindi na Kituruki. Makala haya yanajaribu kutalii mtagusano wa Kiswahili na jamii-lugha nyingine kwa lengo la kuona jinsi lugha hizi zilivyoathiriana kimsamiati. Mtagusano wa Kiswahili na jamii-lugha nyingine umesababisha kuibuka mitazamo mbalimbali kuhusu chimbuko na asili ya Kiswahili. Kuhusu chimbuko, wapo wanaodai kuwa Kiswahili kilianzia sehemu moja na kusambaa sehemu nyingine na wapo wanaodai kuwa Kiswahili kilichimbukia sehemu mbalimbali za upwa wa Afrika Mashariki. Ama kuhusu asili, upo mtazamo unaokiona Kiswahili kama lugha inayotokana na Kiarabu. Vilevile, upo mtazamo unaochukulia Kiswahili kama lugha chotara na upo mtazamo unaodai kuwa Kiswahili ni Kibantu. Sababu za kuzuka kwa mitazamo hiyo ni kuwapo kwa msamiati au miundo yenye asili ya lugha za kigeni katika Kiswahili. Kwa mujibu wa makala haya, kama ambavyo imedokezwa pia na Massamba (2017), kupatikana kwa msamiati mwingi wa kigeni katika Kiswahili haiwi sababu ya Kiswahili kuwa na asili ya lugha hiyo ya kigeni bali ni matokeo ya lugha kuathiriana zinapokutana. Lugha zinapokutana huweza kuathiriana katika viwango mbalimbali kama vile sauti, mofimu, msamiati na sarufi kwa ujumla. Lengo kuu la makala haya ni kubainisha athari za kimsamiati zinazotokana na mtagusano huo wa jamii-lugha ya Waswahili na jamii-lugha nyingine. Aidha, pale ilipobidi athari za kifonolojia zimejadiliwa katika baadhi ya maeneo. Data ya utafiti huu ni ya maktabani. Hivyo, mbinu ya kukusanyia data ya makala haya ni usomaji matini mbalimbali zinazohusu mtagusano wa Kiswahili na lugha nyingine.

## 1.0 Utangulizi

Tunapojadili mtagusano wa jamii-lugha ya Waswahili na jamii-lugha nyingine hatuna budi kutalii japo kwa ufupi juu ya chimbuko la Kiswahili. Lengo la kufanya hivyo ni kupata usuli wa mahali ambapo jamii-lugha hiyo ilianzia na namna

[1] Baruapepe: mumoshe2006@yahoo.com

ilivyosambaa na kukutana na jamii-lugha nyingine. Kumekuwapo na mitazamo mbalimbali kuhusu chimbuko la Kiswahili. Ikumbukwe kuwa chimbuko na asili ya Kiswahili ni vitu viwili tofauti. Massamba, Kihore na Hokororo (2001) wanatubainishia tofauti kati ya chimbuko na asili ya Kiswahili kwa kueleza kwamba tunapoangalia chimbuko la Kiswahili, tunaangalia ni mahali gani Kiswahili kilianzia na kwa upande wa asili tunaangalia ni jinsi gani Kiswahili kilianza. Kwa vile hapa tunaangalia ni kwa namna gani jamii-lugha ya Waswahili imefanya mtagusano na jamii-lugha nyingine, suala la mahali ambapo Kiswahili kilianzia tumelipa kipaumbele zaidi kuliko suala la jinsi Kiswahili kilivyoanza. Suala la kufahamu chimbuko la Kiswahili ni muhimu, kwani litasaidia kujua lugha hiyo imeanzia wapi.

Mtazamo wa kwanza ni ule unaodai kuwa Kiswahili kilianzia sehemu moja na kusambaa katika maeneo mengine. Mbaabu (2007) anaamini kuwa Kiswahili kilianzia pwani ya Kaskazini mwa Kenya, maeneo kati ya Lamu na mahali ambapo Mto Tana unaingia baharini. Hivyo basi, jamii-lugha ya Waswahili ilianzia sehemu moja na kisha kusambaa katika sehemu nyingine. Eneo hilo ndilo analiita ‘uswahilini’ akiamini kuwa ndipo ambapo Waswahili wa mwanzo kabisa walipatikana. Anadai kuwa Kiswahili kilienea upande wa Kusini kuanzia Mombasa mpaka Kilwa na kwa upande wa Kaskazini kilienea mpaka Mogadishu. Kwa hakika mtazamo huu haukuanzia kwa Mbaabu tu, ila kuna watangulizi wake ambao wanaamini kuwa ni muhali lugha kuanzia katika sehemu mbalimbali kwa wakati mmoja. Miongoni mwao ni Nurse na Spear (1985:7) ambao wanasema kuwa:

> … Mtazamo huu wa Kiswahili kuanzia sehemu mbalimbali unakinzana na tunachojua kutoka katika lugha zisizo na idadi ulimwenguni. Lugha huanzia sehemu moja kwa muda fulani. Watumiaji wake huongezeka na lugha huanza hujitofautisha kati ya mzungumzaji na mzungumzaji (lahaja). Jamii inapogawanyika na baadhi ya wazungumzaji wakitawanyika ndio utofauti wa kiisimu unaongezeka” (Tafsiri yangu).

Katika maelezo haya, inaonekana wazi kuwa wanamtazamo huu wanapinga uwezekano wa Kiswahili kuanzia katika pwani yote ya Afrika Mashariki. Wanachoamini ni kuwa Kiswahili kilianzia sehemu moja na kusambaa katika sehemu nyingine. Swali ambalo linaweza kuzuka kuhusu mtazamo huu ni Je, Kiswahili chenyewe kilikuwa kipi na kilianzia wapi na kuenea katika pwani yote ya Afrika Mashariki kabla ya ujio wa wageni? Mbaabu (2007) anataka kutuaminisha kuwa Kiswahili chenyewe ni kile cha Lamu na kilianzia katika Mji wa Lamu. Dai hili linatia mashaka kihistoria, kwani ukilinganisha Mji wa Lamu na miji mingine ya pwani ya Afrika Mashariki kihistoria inaonekana wazi ipo miji iliyoendelea mapema kabla ya Lamu. Massamba (2017) akimnukuu Freeman-Grenville (1959) anasema kuwa rekodi za kihistoria zinaonesha kuwa Mji wa Kilwa ulikuwa maarufu mapema zaidi hata kabla ya Mji wa Lamu. Ikiwa hoja ya Kiswahili ni kwamba kilianzia sehemu moja na kuenea sehemu nyingine za pwani ya Afrika


Mashariki, basi ingekuwa hoja madhubuti kama Mji wa Kilwa ungehusishwa zaidi na sehemu hiyo kuliko Mji wa Lamu.

Mtazamo mwingine kuhusu chimbuko la Kiswahili ni ule unaodai kuwa Kiswahili kilianzia katika sehemu mbalimbali za pwani ya Afrika Mashariki (Chami, 1994 na Massamba, 2017). Wanamtazamo huu wanadai kuwa watu wa sehemu mbalimbali katika pwani hiyo, kuanzia Kaskazini mpaka Kusini walikuwa wakizungumza lugha zao za Kibantu. Kwa vile lugha hizo zilikuwa hazina tofauti kubwa na kutokana na mtagusano wao katika shughuli za kibiashara, walirahisisha lugha zao ili waweze kufanya mawasiliano wao kwa wao. Hali hii ikasababisha kuwapo kwa vilugha (lahaja) mbalimbali katika upwa huu kama vile Chimini, Kiamu, Kimvita, Kipemba na Kiunguja (Massamba na wenzie, 2001 na Massamba, 2017).

Katika makala haya tunakubaliana na mtazamo huu wa pili unaodai kuwa chimbuko la Kiswahili ni sehemu mbalimbali za upwa wa Afrika Mashariki. Dai hili tunaliona lina mashiko zaidi kutokana na sababu kuu mbili. Mosi, lau kama Kiamu kingekuwa ndio chimbuko haswa la Kiswahili, basi lahaja hiyo ingekuwa imesambaa na kuonekana nyepesi kusanifishwa katika pwani ya Afrika Mashariki kuliko Kiunguja. Ikumbukwe kwamba mwaka 1928 kulifanyika mkutano Mjini Mombasa uliowakutanisha wawakilishi kutoka Kenya, Tanganyika, Uganda na Zanzibar (Maganga, 2008). Mkutano huo ulikuwa na lengo la kuteua lahaja moja ya Kiswahili ambayo ingesanifiwa na kutumika katika eneo lote la Afrika Mashariki. Wajumbe wa mkutano huo walikubaliana kuwa Kiunguja kilifaa zaidi kuliko Kimvita na lahaja nyingine yoyote (Mbaabu, 2007). Pili, kama tulivyosema hapo awali kuwa ikiwa Kiswahili kimechimbukia katika sehemu moja tu katika pwani ya Afrika Mashariki, basi Mji wa Kilwa ungekuwa mwafaka zaidi kuliko Lamu kwani ulikuwa maarufu kabla ya Mji wa Lamu. Nurse na Spear (1985) walithibitisha hilo kwa kusema kuwa, umuhimu wa mji wa Kilwa ulihamia Lamu katika karne ya 16 baada ya Wareno kuitawala Kilwa.

Ingawa mjadala wa wapi Kiswahili kimeanzia umekuwa na mvutano kama pande mbili zilivyoonekana hapo juu, kwa mujibu wa makala haya tunahitimisha kwa kuwaunga mkono wale wanaoona kuwa Kiswahili kiliibukia sehemu mbalimbali za pwani ya Afrika Mashariki. Hii ina maana kuwa, wageni walipofika eneo hili waliwakuta wenyeji wakiongea lugha zao (lahaja). Inasemekana baadhi ya lugha hizo zilikuja kujulikana kwa jina la Kiswahili, lenye asili ya Kiarabu likimaanisha pwani ( Polomé, 1967; Ghanem, 1995).

Katika makala haya, tunapozungumzia pwani ya Afrika Mashariki tuna maana ya eneo linaloanzia pwani ya Mogadishu mpaka pwani ya Sofala kama ramani ifuatayo inavyoonesha:




**Kielelezo 1:** Ramani ya Pwani ya Afrika Mashariki
**Chanzo**: Nurse na Spear (1985: 17)

## 2.0 Mtagusano wa Kiswahili na Jamii-Lugha nyingine za Kigeni

Kama ilivyoelezwa hapo awali kuwa chimbuko la Kiswahili ni katika pwani ya Afrika Mashariki; jamii-lugha nyingine kutoka nje ya eneo hili zilifanya mtagusano na wenyeji wa eneo hili. Mtagusano huo umesababisha Kiswahili kuathiri na kuathiriwa na lugha nyingine (Chiraghdin na Mnyapala, 1977). Athari zinazotokana na mtagusano wa lugha mbili au zaidi zinaweza kupatikana katika sauti, msamiati au miundo. Kiswahili nacho kimepata na kutoa athari hizo katika lugha nyingine.

Jamii-lugha ya Waswahili ilivyoingiliwa katika maeneo yake au kusambaa katika maeneo mengine ilijikuta ikitagusana na jamii-lugha nyingine za kigeni. Jamii-lugha nyingi zilizotagusana na Waswahili zilitoka ndani na nje ya Bara la Afrika. Miongoni mwa jamii lugha zilizoathiri Kiswahili hususani katika kiwango cha msamiati ni pamoja na Kireno, Kihindi, Kituruki, Kiarabu, Kijerumani na Kiingereza (Chuwa, 1988; na Lodhi, 2000). Kwa upande mwingine, Kiswahili nacho kimechangia kwa kiasi chake katika kujenga msamiati wa lugha hizo. Mifano ya maneno ya Kiswahili katika lugha hizo ni yale yanayopatikana katika

Kiingereza. Maneno hayo ni pamoja na: *mzee*, *panga*, *shamba* na *safari*[2]. Maneno *shamba* na *safari* inasemekana yana asili ya Kiarabu ila yameingia katika Kiingereza kupitia Kiswahili. Neno *shamba* tumeliingiza kwenye maneno yenye asili ya Kibantu japokuwa Chuwa (1988) anadai kuwa neno hilo linatokana na neno la Kifaransa 'champ' ila liliingia katika Kiswahili kupitia Kiarabu. Dai hili linatia mashaka, kwani neno *shamba* halina dalili ya kuingia katika msamiati wa Kiarabu. Katika lugha hiyo, neno linalotumika kuwakilisha *shamba*ni مزرع /'*mazraҁa'* / au مزارع /mazaariҁ/. Kwa hakika neno hili '*mazraҁa'* ndilo lililotupatia neno la Kiswahili la '*maziara'* likiwa na maana ya mahali panapozikiwa wafu.

Mtagusano wa lugha hizi na Kiswahili unaweza kuwekwa katika makundi mawili ambayo ni mtagusano wa kijamii na mtagusano wa kiutawala. Mtagusano wa kijamii ni ule ambao Waswahili walikutana na kushirikiana na jamii hizo katika miamala mbalimbali pasipo na Waswahili kutawaliwa kisiasa. Aidha, mtagusano wa kiutawala ni ule ambao pamoja na miamala mingine ya kijamii lakini Waswahili walitawaliwa kisiasa na jamii hizo.

### 2.1 Mtagusano wa Kijamii wa Jamii-lugha ya Waswahili na Jamii-lugha za Kigeni

Mtagusano huu unahusisha jamiii-lugha nyingi zisizo za Kibantu ambazo zimekutana na kufanya miamala mbalimbali ya kijamii na jamii-lugha ya Waswahili. Kutokana na jamii-lugha hizo kuwa nyingi, katika makala haya tutatumia mifano michache kutoka jamaii-lugha za Kihindi na Kituruki.

#### 2.1.1 Mtagusano wa Kijamii wa Jamii-lugha ya Waswahili na Wahindi

Jamii-lugha ya Wahindi ambao walikuwa wafanyabiashara wakubwa katika pwani ya Afrika Mashariki, inaaminika ilianza kutagusana na jamii ya Waswahili mwaka 1896[3]. Mtagusano huo kati ya Wahindi na Waswahili ulisababisha Kiswahili kuathriwa kimsamiati na lugha ya Kihindi. Baadhi ya maneno yaliyotoka katika msamiati wa Kihindi na kuingia katika Kiswahili yanapatikana katika Jedwali Na. 01 hapa chini:

**Jedwali Na. 01: Mifano ya Maneno yenye Asili ya Kihindi katika Kiswahili**

| **Na.** | **Neno lenye asili ya Kihindi** | **Ufafanuzi Wake** |
|---|---|---|
| 1 | Asteaste | Taratibu |
| 2 | Basmati | Aina ya mchele mwembamba |
| 3 | Chakari | Kupita kiasi |
| 4 | Kachumbari | Mchanganyiko wa vitu mbalimbali kama vile, nyanya, kitunguu, n.k ambao huliwa pamoja na chakula |
| 5 | Mamsapu | Mke wa mtu aliyekuajiri |

**Chanzo:** BAKITA (2021)

[2] Maneno haya yanapatikana katika *Oxford Advanced Learner's Dictionary* (Toleo Jipya la 8)
[3]*En.wikipedia.org/wiki/East_Africa_Protectorate* (14.05.2003: 5:15 asubuhi)

Orodha ya maneno katika Jedwali Na. 01 ni baadhi ya maneno yenye asili ya Kihindi yaliyoingia katika msamiati wa Kiswahili. Kutokana na Wahindi kujihusisha sana na biashara inaonekana kuwa sehemu kubwa ya maneno hayo pia yanatokana na uga wa biashara na ajira. Maneno hayo yanahusu majina ya vyakula kama vile *mchele* na *kachumbali*. Vilevile, yapo yanayohusu idadi au kiasi cha vitu au hali ambayo ni kama vile *asteaste* na *chakari*.

### 2.1.2 Mtagusano wa Kijamii wa Jamii-lugha ya Waswahili na Waturuki

Inaelezwa kuwa jamii- lugha ya Waswahili ilikutana na Waturuki katika Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia zikiwa chini ya mamlaka ya Ujerumani[4].; kutokana na mtagusano huo jamii hizi mbili kumesababisha Kiswahili kukopa maneno kutoka katika Kituruki haswa istilahi za kijeshi Chuwa (1988). Baadhi ya maneno yenye asili ya Kituruki yaliyoingia katika msamiati wa Kiswahili umo katika Jedwali Na. 02.

**Jedwali Na. 02: Mifano ya Maneno yenye Asili ya Kituruki katika Kiswahili**

| Na. | Neno lenye Asili ya Kituruki | Ufafanuzi Wake |
|---|---|---|
| 1 | Afande | Jina la mtu mwenye cheo katika jeshi |
| 2 | Askari | Mtu anayejishughulisha na ulinzi wa raia na mali zao |
| 3 | Bimbashi | Afisa wa jeshi mwenye cheo chini ya lutein |
| 4 | Bishaushi | Cheo cha askari mzawa wakati utawala wa Wajerumani |
| 5 | Tapo | Kikundi cha watu |

**Chanzo:** BAKITA (2021) na Chuwa (1988)

Jedwali Na. 02 limebainisha baadhi ya maneno yenye asili ya Kituruki yaliyoingia katika msamiati wa Kiswahili. Kwa namna yalivyo maneno hayo, ni dhahiri kuwa yamefungamana na muktadha wa kijeshi.

## 2.2 Mtagusano wa Kiutawala wa Jamii-lugha ya Waswahili na Jamii za Kigeni

Jamii-lugha zilizofanya miamala ya kiutawala na Waswahili zipo nne ambazo ni: Wareno, Waarabu, Wajerumani na Waingereza. Pamoja na jamii zote hizi nne kutagusana na jamii-lugha ya Wiswahili, inaaminika kuwa Waarabu na Waingereza ndio walioacha athari kubwa ya kimsamiati katika lugha ya Kiswahili (Lodhi, 2000). .

### 2.2.1 Mtagusano wa Jamii-lugha ya Waswahili na Waarabu

Waarabu[5] walianza kufanya mtagusano na wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki katika karne za mwanzoni kabisa (Polomé, 1967; Nurse na Spear, 1985; na Lodhi,

[4] www.thenagain.info/web Chron/ East Europe/ *Truckey Central. html*. (29.06.2020: 6:32 mchana)

[5] Waarabu kwa mujibu wa makala haya ni wale wote waliotoka Ghuba ya Urabuni (*ArabianGulf*) ambao watakuwa ni Waomani, Washirazi n.k.

2000). Kwanza kabisa, walianza na mtagusano wa kibiashara, ambapo walileta nguo, zana za chuma na shanga na wao walichukuwa dhahabu, mbao na watumwa. Inasemekana walikuwa wakija kila mwaka kwa kutumia Pepo za Kaskazi na kurudi na Pepo za Kusi (Nurse na Spear, 1985).

Mara baada ya kufanya biashara kwa muda mrefu katika eneo hili, Waarabu walivutiwa na kutaka kulitawala eneo hili. Nurse na Spear (1985) wanadai kuwa mwishoni mwa Karne ya 17 Sultani wa Oman aliwaondoa Wareno katika maeneo yaliyokaliwa na Waswahili katika pwani ya Afrika Mashariki na kuanzisha utawala wake huko Zanzibar. Kuwapo kwa utawala wa sultani katika pwani ya Afrika Mashariki kulisababisha kuongezeka kwa mtagusano wa Waarabu na Waswahili (Ade-Ajayi, 1999). Mtagusano huu wa Waarabu na Waswahili ulisababisha Kiswahili kisiepuke kuathiriwa na Kiarabu katika viwango mbalimbali. Mathalani, katika kiwango cha kifonolojia, Kiswahili kimekopa sauti za Kiarabu na kuzifanya kama za kwake. Kuna sauti kama vile ث***/th/***, ذ***/dh/***, غ ***/gh/*** *na* خ ***/kh/*** ambazo zinatumika katika Kiswahili na kuonekana kama zina asili na lugha hiyo. Hata ikitokea unataka kuzibadili na sauti zilizokuwapo katika Kiswahili unaweza kubadilisha maana ya kile ulichokusudia. Mathalani, neno *thamani* ukitaka kusema *samani* utakuwa na maana mbili tofauti. Neno la kwanza lina maana ya *gharama au ubora wa kitu* na lile la pili, lina maana ya *vyombo vya nyumbani au ofisini kama vile meza, viti, kabati na vitanda*.

Inasemekana kuwa Kiswahili kimeathiriwa sana kimsamiati na Kiarabu kiasi kwamba kimepokea maneno mengi kutoka katika Kiarabu (Bosha, 1994; na Lodhi, 2000). Nurse na Spear (1985) wanadai kuwa Kiswahili kina zaidi ya asilimia 50 ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika nyanja za sheria, biashara, dini, mimea asilia na shughuli za uvuvi. Dai hilo limetiliwa mkazo na Lodhi (2000) aliposisitiza kuwa Kiarabu kinaongoza kwa kuchangia msamiati katika Kiswahili haswa katika fani za biashara, fasihi, dini na sheria. Kumekuwapo na tofauti za kiidadi katika maneno ya mkopo katika Kiswahili. Hali hii inasababishwa na kila mtafiti kutumia vyanzo tofauti vya data. Mathalani, Mohamed (2010) kwa kutumia KKS (Toleo la 2) anadai kuwa kuna jumla ya asilimia 19 ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili katika nyanja anuai. Japokuwa suala la idadi ya maneno ya Kiarabu katika Kiswahili limekuwa na mvutano mkubwa lakini jambo ambalo wanaisimu wanakubaliana pasipo ubishi ni kuwa Kiswahili kimekopa maneno katika Kiarabu. Suala la idadi linahitaji utafiti zaidi. Mifano ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili inapatikana katika Jedwali Na. 03 lifuatalo:

**Jedwali Na. 03: Mifano ya Maneno yenye Asili ya Kiarabu katika Kiswahili**

| **Na.** | **Neno lenye Asili ya Kiarabu** | **Ufafanuzi wake** |
|---|---|---|
| 1. | Bazazi | 1. Mtu atumiaye hila. Mlaghai<br>2. Mzururaji (Pemba) |

| Na. | Neno lenye Asili ya Kiarabu | Ufafanuzi wake |
|---|---|---|
| 2. | Hani | 1Toa pole kwa mfiwa<br>2. Pongeza |
| 3. | Hawara | Mwanamke au mwanamume anayekaa na mtu asiyeoana naye, kimada, bibi |
| 4. | Hayati | Marehemu |
| 5. | Liwaza | Bembeleza ili kutoa mtu majonzi, fariji. |

**Chanzo**: Shembilu (2017).

Maneno yaliyomo katika Jedwali Na. 03 ni baadhi tu ya maneno lukuki yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili. Maneno hayo matano pia yanawakilisha orodha kubwa ya maneno yenye asili ya Kiarabu ambayo yameingia katika Kiswahili kwa kugeuzwa au kubadilishwa maana zake. Neno kama vile *hayati* katika Kiswahili maana inayotumika kumuita mtu aliyekufa, yaani marehemu, ilhali katika Kiarabu linatumika kwa maana ya uhai au maisha.

Kutokana na mtagusano huo na idadi kubwa ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili kumeibuka kundi linalodai kuwa Kiswahili ni Kiarabu. Kwa hakika wingi wa maneno ya mkopo katika lugha hausababishi lugha kopaji kupoteza uasili wake. Si Kiswahili tu chenye maneno mengi ya mkopo, bali zipo lugha nyingi duniani ambazo msamiati wake umesheheni maneno ya mkopo. Mathalani, Kiingereza kina maneno mengi kutoka lugha za Kifaransa, Kijapani, Kigiriki na Kilatini. Hatuwezi kusema kuwa Kiingereza kiitwe Kifaransa kwa kuwa kina msamiati mwingi wa Kifaransa (Nurse na Spear, 1985; Lodhi, 2000).

Kuafikiana na madai ya kukihusisha Kiswahili ni Kiarabu kwa kuwa kina msamiati mwingi wenye asili ya Kiarabu ni kujiweka hatarini. Hatari yenyewe ni kuwa ipo siku tutakiona Kiswahili ni Kiingereza, kwani inasemekana kuwa kwa sasa Kiingereza kinakuja kwa kasi katika kuchangia msamiati wa Kiswahili haswa katika nyanja za sayansi na teknolojia (Lodhi, 2000). Kwa hakika Kiswahili na Kiarabu ni lugha mbili zenye asili tofauti kabisa. Kiswahili kina asili ya Kibantu[6]na Kiarabu kina asili ya Kisemitiki; hivyo, hatuwezi kusema kuwa Kiswahili kina asili ya Kiarabu (Bosha, 1994). Vilevile, kwa kuangalia kigezo cha sarufi ya lugha, Kiswahili kina vionjo vyote vya Kibantu kuliko vile vya Kiarabu na lugha nyingine haswa katika mpangilio wa viambajengo vyake.

### 2.2.2 Mtagusano wa Jamii-lugha ya Waswahili na Wareno

Inasemekana kuwa Wareno walitamalaki katika upwa wa Afrika Mashariki kwenye nusu ya pili ya Karne ya 15 mpaka walipotimuliwa na Waarabu katikati ya Karne ya 17 (Polome, 1967). Bosha (1994) anadai kuwa Wareno walitamalaki pwani ya

[6] Ithibati za Ubantu wa Kiswahili zinapatikana katika Massamba na wenzie (2001).

Afrika Mashariki kwa zaidi ya miaka 190. Pamoja na kuwa na mtagusano na eneo la pwani ya Afrika Mashariki kwa miaka mingi, Kireno kimeingiza kiasi kidogo cha msamiati ukilinganisha na lugha nyingine zilizokuwa na mtagusano na eneo hili kama vile Kiingereza na Kiarabu. Sababu kubwa ya Kireno kutoingiza msamiati mwingi katika Kiswahili ilitokana na kuwapo kwa uhusiano mbovu au wa kimabavu baina ya Wareno na Waswahili. Kwa mujibu wa Nurse na Spear (1985), Wareno walipofika katika Pwani ya Afrika Mashariki waliharibu miji ya wenyeji kwa lengo la kutawala biashara katika Bahari ya Hindi. Jambo hili kwa hakika halikuleta muamala mzuri baina ya wenyeji na Wareno. Vilevile, namna walivyoshugulikia watumwa na kueneza dini ya kikristo kwa wenyeji ambao wengi wao walishaingia katika uislamu, kulisababisha wenyeji kutowapenda Wareno.

Miongoni mwa sababu ya lugha moja kukopa msamiati kutoka lugha nyingine ni suala la watumiaji wa lugha kopaji kujifaharisha kutumia msamiati wa lugha inayokopwa. Kutokana na Wareno kutokuwa na uhusiano mzuri na wakazi wa Pwani ya Afrika Mashariki, wakazi wake hawakuona fahari kutumia maneno ya Kireno. Baadhi ya maneno yaliyoingia katika msamiati wa Kiswahili yanapatikana katika Jedwali Na. 04 hapa chini:

**Jedwali Na. 04: Mifano ya Maneno yenye Asili ya Kireno katika Kiswahili**

| Na. | Neno lenye Asili ya Kireno | Ufafanuzi Wake |
|---|---|---|
| 1 | Bendera | Kitambaa chenye rangi, alama au nembo maalumu inayotambulisho nchi au chama. |
| 2 | Bibo | Tunda la mkanju, tunda la mkorosho |
| 3 | Danguro | Nyumba ambamo shughuli za umalaya hufanywa. |
| 4 | Karata | Kadi inayotumika katika mchecho kama vile arubastini. |
| 5 | Meza | Samani inayoundwa kwa mbao, chuma au vifaa vingine, agh. hutumika kwa kuandikia |

**Chanzo:** TUKI (2018) na BAKITA (2021).

Mifano ya maneno katika Jedwali Na. 04 ni ya Nyanja mchanganyiko, ambapo kuna ya vifaa kama vile *meza*, *karata* na *bendera*, matunda kama vile bibo na maeneo ya starehe kama vile *danguro*. Huenda hali hii imesababishwa na Wareno kujihusisha na shughuli mbalimbali kama vile, utawala, biashara na kueneza dini.

### 2.2.3 Mtagusano wa Jamii-lugha ya Waswahili na Wajerumani

Wajerumani walikuwa wageni waliofuatia kufanya mtagusano wa kiutawala na Waswahili baada ya Waarabu. Inasemekana Wajerumani walihimiza matumizi ya Kiswahili katika shule zao na kujua Kiswahili lilikuwa sharti muhimu la kufanya kazi na utawala wa Kijerumani (Massamba na wenzie, 2001). Wajerumani

waliamua kufundisha Kiswahili katika ngazi ya chini ya elimu ili kupata wafanyakazi katika utawala wao. Vilevile, uhimizaji mkubwa wa matumizi ya Kiswahili uliofanywa na Wajerumani ulitokana na kutaka kukubaliwa kwao kirahisi na wenyeji haswa baada ya kushindwa kwa sera yao ya kukuza Kijerumani. Bosha (1994) anadai kuwa Wajerumani wametawala baadhi ya sehemu za Afrika Mashariki kwa zaidi ya miaka 30. Hata hivyo, pamoja na kutamalaki katika eneo hili kwa kipindi hicho, Kijerumani kimechangia maneno katika Kiswahili kwa kiasi kidogo. Kupatikana kwa maneno machache yenye asili ya Kijerumani katika Kiswahili huwenda kumetokana na Wajerumani kuweka msisitizo katika matumizi ya Kiswahili katika utawala wake. Jedwali Na. 05.linabainisha baadhi ya msamiati wa Kijerumani ulioingia katika Kiswahili.

**Jedwali Na. 05: Mifano ya Maneno yenye Asili ya Kijerumani katika Kiswahili**

| **Na.** | **Neno lenye Asili ya Kijerumani** | **Ufafanuzi Wake** |
|---|---|---|
| 1 | Buruda | Mtawa mwanaume wa madhehebu ya Kikatoliki |
| 2 | Hela | Noti au sarafu halali iliyoidhinishwa na serikali |
| 3 | Shule | Mahali penye majengo ambapo wanafunzi hufundishwa |

**Chanzo:** BAKITA (2021) na Chuwa (1988)

Data katika Jedwali Na. 05 inaonesha kuwa msamiati huo wenye asili ya Kijerumani umejigawa katika Nyanja tatu ambazo ni dini, uchumi na elimu. Nyanja hizo zilikuwa muhimu sana katika utawala wa Wajerumani.

### 2.2.4 Mtagusano wa Jamii-lugha ya Waswahili na Waingereza

Waingereza walikuwa na mtagusano na watu wa Afrika Mashariki tangu miaka ya 1880. Inasemekana katika kipindi hicho kulikuwa na Waingereza waliokuwa wakifanya kazi pamoja na utawala wa sultani. Miongoni mwa Waingereza hao ni Bw. John Kirk aliyekuwa mshauri mkuu wa Sultani Barghash bin Said na Lloyd Methew aliyekuwa kamanda wa jeshi la Sultani. Mtagusano wa kiutawala na jamii ya Waswahili haswa wa Tanganyika na Zanzibar ulifanyika mara baada ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia ambavyo vilitokea kati ya mwaka 1914 na 1918 (Parpart na Rostgaard, 2006).

Inadaiwa kuwa katika wakoloni waliopata kutawala eneo hili la Afrika Mashariki, Waingereza walifanya juhudi kubwa zaidi za kukikuza na kukieneza Kiswahili. Juhudi za kukikuza Kiswahili hazikutokana na Waingereza kuipenda sana lugha hii kuliko Kiingereza, bali walilazimika kufanya hivyo kutokana na hali halisi ya matumizi ya Kiswahili ya wakati huo. Kipindi cha utawala wa Waingereza ndipo lahaja ya Kiunguja iliposanifishwa na kupatikana kwa Kiswahili sanifu tunachotumia leo hii (Mbaabu, 2007; Maganga, 2008 na Massamba, 2017).

Kutokana na mtagusano huu wa Waingereza na Waswahili wa Afrika Mashariki, imekuwa ni sababu ya Kiingereza kukiathiri Kiswahili katika viwango mbalimbali vya kisarufi kama vile fonolojia na msamiati. Baadhi ya athari za kifonolojia za Kiingereza katika Kiswahili ni baadhi ya mkururo wa sauti za Kiingereza kupatikana katika Kiswahili. Mathalani, katika Kiswahili kuna mkururo wa sauti kama vile *skr* katika neno **skrubu** ambalo linatokana na neno la Kiingereza 'screw', *skw* katika neno **skwea** linalotokana na neno 'square' na *dr* katika neno **haidroliki** linalotokana na neno 'hydrolic'. Kwa hakika mkururo huu wa *skr*, *skw* na *dr* haupatikani katika maneno yenye asili ya Kibantu isipokuwa umeingia katika Kiswahili kutoka katika Kiingereza.

Kama ilivyokwishaelezwa, Kiswahili kimekopa maneno mengi kutoka katika Kiingereza hususani katika tasnia ya sayansi na teknolojia (Lodhi, 2000). Hali hii imetokana na ukweli kuwa vifaa vingi vya kiteknolojia vinavyoingia katika jamii-lugha ya Waswahili huingia na majina yake. Waswahili hulazimika kukopa maneno kutoka katika Kiingereza sio kwa ufahari tu bali wakati mwingine ni kwa ajili ya kuziba pengo la kimsamiati lililopo. Mbali na msamiati wa sayansi na teknolojia kuwa mwingi katika Kiswahili, upo pia msamiati wa maneno ya kawaida ambao dhana yake ilikuwa ngeni katika Kiswhaili. Mifano ya msamiati wa Kiswahili uliokopwa kutoka katika Kiingereza unapatikana katika Jedwali Na. 06:

**Jedwali Na. 06: Mifano ya Maneno yenye Asili ya Kiingereza katika Kiswahili**

| Na. | Neno lenye Asili ya Kiingereza | Ufafanuzi Wake |
|---|---|---|
| 1. | ajenda | 1. Orodha ya mambo yatakayozungumzwa kwenye mkutano.<br>2. Nia/ lengo |
| 2. | batiza | 1. Tia mtu maji katika ibada ya kumpokea katika dini ya kikristo.<br>2. –pa jina si lake. |
| 3. | gauni | Kanzu au vazi refu livaliwalo na wanawake |
| 4. | yunifomu | sare |
| 5. | lofa | 1. Mtu anayezururazurura asiye na kitu wala kazi.<br>2. Mtu masikini/mwenye kipato kidogo<br>3. Mtu asiyeelewa |

**Chanzo:** Shembilu (2017)

Jedwali Na. 06 linabainisha baadhi ya mifano ya maneno yaliyokopwa kutoka Kiingereza na kuingizwa katika Kiswahili. Mathalani, neno *batiza* ni miongoni mwa maneno ambayo dhana yake ilikuwa ngeni katika Kiswahili; hivyo, ilibidi neno hilo liingie na fahiwa zake. Kitendo cha kumtumbukiza mtu majini kwa lengo la 'kumuingiza' katika Ukristo hakikuwapo katika jamii-lugha ya Waswahili kwani baadhi ya Waswahili walikuwa wameshaingia katika Uislamu na wengine

walikuwa katika dini zao za jadi. Inasadikiwa kuwa wageni wa mwanzo kuleta Ukristo ni Wareno na waliingia katika karne ya 16. Ikumbukwe kuwa pamoja na Wareno waliondolewa na Waarabu katika karne ya 17, Waarabu hao walikuwa tayari wana mtagusano na watu wa Afrika Mashariki katika karne za mwanzo kabisa (Polomé, 1967 na Nurse na Spear, 1985).

## 3.0 Hitimisho

Makala haya yamechunguza masuala mbalimbali yanayotokana na mtagusano wa jamii-lugha ya Wiswahili na jamii-lugha nyingine. Makala yamejaribu kubainisha baadhi ya jamii-lugha zilizotagusana na Kiswahili katika miamala ya kijamii na kiutawala. Imebainika kuwa katika mtagusano huo kumekuwapo na kuathiriana kimsamiati baina ya jamii-lugha ya Waswahili na jamii-lugha nyingine, kama vile Waaarabu, Wareno, Wajerumani, Waingereza, Wahindi, na Waturuki[7]. Lugha ambazo zimeonekana kuwa na mchango mkubwa kimsamiati kwenye Kiswahili ni Kiingereza na Kiarabu katika nyuga za sayansi na teknolojia na fasihi na biashara mtawalia (Lodhi, 2000). Aidha, imedhihirika pia kwamba kutokana na mwingiliano baina ya Kiswahili na Kiingereza hususani katika ukanda wa Afrika Mashariki, lugha ya Kiingereza ina maneno iliyoyakopa kutoka katika Kiswahili. Jambo hili la kuongezeka kwa msamiati wa Kiswahili katika Kiingereza linatuonesha jinsi Kiswahili kinavyokua na kukubalika katika jamii-lugha nyingine.

## Marejeleo


Ade Ajayi, F. (1999) *Historia Kuu ya Afrika VI*: *Afrika kwenye Karne ya 19 hadi Miaka ya 1980*. (Toleo lililofupishwa) Dar es Salaam: TUKI.

BAKIZA (2021) *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (Toleo la 3). Nairobi: Longhorn Pupblisher Limited

Bosha, I. (1994) *The Influence of Arabic Language on Kiswahili with Trilingual Dictionary* (*Swahili- Arabic- English*). Dar es Salaam: DUP.

Chami, F A. (1994) *The Tanzanian Coast in the First Millenium AD: An Archeology of the Iron-Working, Farming Communities*. Upsala: Societas Archeologica Upsaliensis.

Chiraghdin, S na Mnyapala, M. E. (1977) *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Chuwa A. R. (1988) “Foreign Loan Words in Kiswahili”. *Kiswahili*, Juzu. 55(1 na 2):168 – 172.

Ghanem, K. S. M. (1995) *Lexical Relatedness between Kiswahili and Arabic*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.


[7] Lugha nyingine kama Kichina zinazoendelea na mtagusano wa kijamii na kibiashara zitajadiliwa katika makala fuatizi.

Kiango, J.G. (2005). “Swahilization of Coastal Bantu Languages: The Case of Bondei Language” (Haijachapishwa). *Makala yaliyowasilishwa katika Warsha ya LOT*, Mei 20 – 22, Dar es Salaam.

Lodhi, A. (2000) *Oriental Influences in Swahili: A Study in Language and Culture Contacts,* Göteborg: Acta Universitis Gothoburgensis.

Maganga, C. (2008) “Maendeleo ya Matumizi ya Kiswahili Tanzania Bara”. Katika J. G. Kiango (Mh.) *Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. Kur. 30-34.

Massamba, D. P. B. (2017) *Historia ya Kiswahili: Mtazamo Mpya 100KK hadi 2000***.** Dar es Salaam: Kiswahili Development Limited.

Massamba, D. P. B, Kihore, Y. M. na Hokororo, J. I. (2001) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbaabu, I. (2007) *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mohamed, M. (2010) *A Study of Adaptation of Arabic Loanwords in Swahili Dictionary: A Case of Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI 2004)*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Nurse, D. na Spear, T. T. (1985) *The SWAHILI: Reconstructing the History of an African Society, 800 – 1500*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Oxford (2010) *Oxford Advanced Learner’s Dictionary, International Student’s Edition*. New York: OUP.

Parpart, J. L. na Rostgaard, M. (Wah.) (2006) *The Practical Imperialist: Letters from A Danish Planter in German East Africa, 1888 – 1906*. Leiden: Brill Academic Publishers.

Polomé, E (1967) *Swahili Language Handbook*. Washington DC: Centre for Applied Linguistics.

Shembilu. M, M (2017) *Michakato ya Kisemantiki ya Maneno Mkopo katika Kiswahili: Mifano kutoka katika Kiingereza na Kiarabu*. Tasnifu yaUzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

TUKI (2018) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 4). Nairobi: Oxford University Press.